



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**



Tarehe: 06/01/2022

**TANGAZO LA AJIRA YA MKATABA YA KAZI ZA UFUNDI KWA AJILI YA UJENZI
WA SHULE MPYA YA MSASANI**

ZABUNI NA. LGA/071/2021/2022/RDC/W/16

1. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe anawatangazia wananchi wote kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe imepokea fedha kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa Miundo mbinu ya Shule mpya ya Sekondari Msasani.
2. Hivyo basi, Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya inakaribisha kazi za Mikataba ya Muda Mfupi za Mafundi wenye sifa na uzoefu katika shughuli za Ujenzi wa Miundo mbinu ya Serikali kwa ajili ya Ujenzi wa Miundo mbinu mbalimbali ya Shule mpya ya Sekondari ambao utafanyika kwa njia ya Manunuzi ya "Force Account" katika fani zifuatazo:-
 - i. Fundi Uashi (ambao utajumuisha upakaji wa rangi, Ufundi umeme na mifumo ya maji safi na taka, uvunaji wa maji safi)
 - ii. Fundi Aluminium (utengenezaji wa madirisha ya Aluminium na milango ya alco bond).
 - iii. Fundi Seremala (inahusisha utengenezaji wa milango na fremu za milango).
 - iv. Fundi kuchomelea vyuma (ambao utajumuisha kutengeneza magrill ya milango na madirisha).
 - v. Fundi wa Mifumo ya Maabara
 - vi. Fundi wa Mifumo ya TEHAMA

Sifa za muombaji

- i. Awe Mtanzania mwenye umri kuanzia miaka 18 na kuendelea
- ii. Awe na Namba ya Utambulisho wa Ulipaji Kodi (TIN)
- iii. Awe na akaunti kwenye benki yeyote iliyopo ndani ya Rungwe

- iv. Awe na ujuzi wa kusoma ramani na kuelezea.
- v. Awe na uzoefu wa kufanya kazi za ujenzi za serikali na mwenye uelewa na taratibu zake. Aambatanishe nyaraka muhimu ili kuthibitisha uzoefu wake katika kufanya kazi za Serikali (yaani aambatanishe nakala za barua za tuzo za kazi alizowahi kufanya, nakala za mikataba ya kazi za ujenzi, nakala za Hati za Malipo za kuanzia mwaka 2018 hadi mwaka 2021).
- vi. Mwombaji awe na uwezo wa kifedha (Mtaji) wa kuwalipa mafundi wake wasaidizi pasipo kuomba kulipwa malipo ya awali (Advance Payments); na kwa msingi huo aambatanishe na taarifa za kibenki (Bank Statement) angalau ya mwaka mmoja (1).
- vii. Awe mzalendo na mwenye kujituma katika kazi.
- viii. Awe na Elimu angalau cheti cha ufundi

KAZI ZITAKAZO FANYIKA KATIKA

1. Kujenga vyumba vya madarasa 8
2. Kujenga maabara za sayansi 3
3. Kujenga jengo la Utawala
4. Kujenga chumba cha TEHAMA (ICT)
5. Kujenga matundu 10 ya Wasichana na 10 ya wavulana
6. Kujenga nguzo ya kuweka tanki la maji lenye ujazo wa lita 10,000
7. Kujenga nyumba za walimu
8. Kujenga miundo mbinu ya kunawa mikono

Aidha, pia Mwombaji anapaswa kuzingatia masharti yafuatayo:-

- a) Mwombaji lazima aandike barua ya maombi kwa jina lake binafsi au kwa jina la biashara akiainisha kazi anayokusudia kujenga/kutengeneza.
 - b) Mwombaji aambatanishe barua ya utambulisho kutoka ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa.
 - c) Mafundi watakaobahatika kupata kazi watalazimika kuajiri mafundi wasiopungua 2 wenye uwezo na uzoefu, wasaidizi wa kutosha kwa kadri ya ukubwa wa kazi husika.
 - d) Awe tayari kufanya kazi muda wote hadi hapo mradi utakapokamilika bila visingizio.
3. Barua za maombi zikiwa zimeambatanishwa na nyaraka tajwa hapo juu katika upande wa sifa na masharti ziwawasilishwe ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kata ya Msasani, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, S.L.P 148, Tukuyu yakiwa yamefungwa vizuri kwenye bahasha nyuma ya bahasha ikitaja jina la kazi inayoombwa.

4. Mwisho wa kupokea maombi ya kazi tajwa hapo juu ni tarehe 13/01/2022 saa 4:00 Asubuhi. Aidha, maombi yatakayoletwa baada ya hapo hayatakubaliwa.
5. Waombaji wote wanatakiwa kuhudhuria usaili wa mafundi/kampuni utakaofanyika tarehe 13/01/2021 saa 4:30 asubuhi tafadhali zingatieni muda huu.
6. Wako katika Ujenzi wa Taifa,


Castory Makeula

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**

**AKURUGENZI MTENDAJI (W)
RUNGWE**